

# TAARIFA KWA VYOMBO VYA HABARI

25 Septemba 2010

## MATUMIZI YASIYO YA LAZIMA KUONGEZEKA KUFIKIA TSH.537 KWA MWAKA WA FEDHA 2010/11

Pamoja na ufinyu wa bajeti ya taifa, kuna baadhi ya vipengele katika bajeti hii ambavyo vinaonekana kuwa havina tija kutokana kwamba haviwanufaishi watanzania walio wengi.

Ni bahati kwamba serikali pia inalitambua tatizo hili la matumizi yasiyo ya lazima kwa wananchi walio wengi na kupitia viongozi wa juu wa Serikali kama Waziri Mkuu, Mh. Mizengo Pinda, ilidhamiria kuongeza udhibiti wa matumizi hayo.

Jumla ya matumizi yote yasiyo ya lazima katika Wizara, Idara na Taasisi za Serikali yalipungua kutoka shilingi za kitanzania bilioni 684 katika mwaka wa fedha wa 2008/09 hadi shilingi za kitanzania bilioni 530 katika mwaka wa fedha 2009/10, ambapo ni punguzo la asilimia 22.4. Lakini, kwa mwaka wa fedha 2010/11. Matumizi haya yasiyo ya lazima yanategemea kuongezeka kidogo na kufikia kiasi cha shilingi za kitanzania bilioni 537, hatua ambayo inapingana na dhamira ya serikali ya kudhibiti matumizi yasiyo ya lazima.

Baada ya kugundua udhaifu katika upangaji na utekelezaji wa bajeti ya serikali, sikika kwa kushirikiana na Policy Forum waliona ni vyema kuandaa toleo la pili la muhtasari wa sera juu ya matumizi yasiyo ya lazima na umuhimu wa serikali wa kuangalia upya jinsi inavyotumia rasilimali zake. Toleo hilo linapatikana katika tovuti [www.sikika.or.tz](http://www.sikika.or.tz). Muhtasari huu utapatikana kwa lugha ya Kiswahili na Kiingereza, na toleo la kwanza la muhtasari huu lilitolewa Aprili 2010.

Muhtasari huu unalenga katika vipengele sita vya bajeti ambavyo vinaonekana kuwa ni matumizi yasiyo ya lazima, ambavyo ni : - mafunzo (ndani na nje ya nchi), Posho (zisizo za hiari na za hiari), Safari ( ndani ya nchi na nje ya nchi), Ununuzi wa magari mapya ya serikali, mafuta ya magari, Mafuta ya kulainisha mitambo na vifaa na huduma za ukarimu'

Pia, muhtasari huu unaelezea kwa kifupi jinsi mgawanyo wa bajeti kuu na ya mikoa inavyobadilika katika vipengele hivyo sita kwa kipindi cha miaka mitatu ya bajeti iliyopita na pia kama mabadiliko hayo yanaendana na maazimio ya Waziri Mkuu na Waziri wa Fedha na Uchumi

Akilizungumzia hilo, mkurugenzi wa Sikika ndugu Irenei Kiria alisema, "Tunaamini kwamba muhtasari huo utaenda kutumika kama wito kwa serikali kusimamia dhamira yake ya kuzuia matumizi yasiyo ya lazima kwa faida ya walipa kodi na kuelekeza fedha hizo katika miradi ya Maendeleo".

MWISHO